BIBLIA KWA TASWIRA, AGANO LA KALE, KITABU CHA 12
Walawi, Sehemu ya Pili

MAMBO YALIYOPITA, YA SASA, NA YANAYOKUJA YA WATU WACHAGULIWA WA MUNGU

(VISUALIZED BIBLE, Vol 12, OT, Past, Present & Future of God's Chosen People)
Mwandishi: Arlene S. Piepgrass
Muchapaji: Vernon Henkel
Imegeuzwa kwa Swahili Congo na watumishi wa Mungu katika DR Congo

© Bible Visuals International
PO Box 153, Akron, PA 17501-0153
Simu: 717-859-1131
www.biblevisuals.org

SOMO 1 - KARAMU ZA BWANA (Sehemu 1)

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Walwi 23:1-14; Kutoka 12; mashairi yaliyo katika somo.

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba Mungu aliagiza Israeli kuangalia siku fulani za Karamu zilizotajwa hata watakumbuk maneno yote ambayo aliwafanyia.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Mungu alipenda watu wake kumushukuru juu ya uangalifu, ulinzi, utoaji wa vifaa, na uongozi wake.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Kusudia kuishi maisha ya kupendeza Mungu.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kutambua maisha yao na kushindana na maneno isiyopendeza Mungu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Siku ya Sabato (Walawi 23:2-3; Mwanzo 2:1-3.)
2. Siku ya Pasaka (Walawi 23:4-5; Kutoka 12:1-51; Torati 16:1-8.)
3. Karamu ya Mukate Usiotiwa Chachu (Walawi 23:6-8; Kutoka 12:14-20.)
4. Karamu ya matunda ya kwanza (Malimbuko) (Walawi 23:9-14; 1 Wakorinto 15:20-23.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mimi ni Bwana Mungu wenu… Mutashika amri zangu zote, na hukumu zangu zote; na kuzitenda: Mimi ni Bwana." Walawi 19:36b-37

Maelezo kwa mwalimu:

Masomo haya pamoja na masomo ya volume 11 ni moja. Masomo haya yatakuwa na faida kuliko kama utayafundisha nyuma ya vitabu 5 vya Kutoka. Masomo katika Kutoka yanakupatia historia kwa maelezo yanayotolewa kwa Israeli katika Walawi. Masomo ya walawi yanakurudisha kwa matokeo katika Kitabu cha Kutoka, hivi yanakupatia njia ukumbusho kwa wanafunzi wako.

Kama ukiwa na Biblia Scofield ujifunze mafundisho juu ya karamu chini ya karasa 220-224. Katika mafundisho ya mbele, tulijifunza juu ya siku za karamu takatifu Mungu alizoagiza watu wake kuchunga.

Karamu hizi zina makusudi mawili: (1) Zilikumbusha Waisraeli saa zte juu ya Mungu, na maneno ambayo aliwafanyia. (2) Ziliwaonyesha mbele maneno amabayo Mungu aliyokusudi kufanya. Mambo haya mengi yamekwisha kutimizwa, lakini mengine yangali kutukia. Ukumbushe wanafunzi kidogo mafundisho ya volume 11. Zungumuza juu ya matoleo, makuhani, sheria kwa maisha ya kila siku, na Siku ya Malipo mbele ya kuanza somo hili.

Somo: Kila mutu anapenda siku kuu. Taja siku kuu sisi tunazokumbuka. (Acha wanafunzi kutaja siku nyingine munazokumbuka katika incho yako. Zungumuza juu ya sababu ya kuzikumbuka na namna kila moja inavyoshikwa. Onyesha ya kuwa siku hizi zinatusaidia kukumbuka mutu fulani ao tokeo lililotukia zamani.)

Waisraeli walikuwa taifa chaguliwa la Mungu. Musa alikuwa kiongozi Mungu aliyechagua kwa taifa lake. Kwa njia ya Musa, Mungu alitoa amri kwa watu kutii. Mungu alieleza vilevile:

(1) Namna watu wa israeli walivyoweza kuja kwake katika damu ya zabihu.
(2) Namna ya kumwabudu
(3) Namna ya kuishi kila siku kumupendeza.

Mungu alitaka watu wake wakumbuke nini ambayo aliwafanyia. Alisema, "Musa, sema na watu kushika karamu takatifu saba. Sharti kila mutu aweke siku hizi kila mwaka. Watu watakutana na kuabudu. Watatoa shukrani na sifa kwa yote ambayo niliwafanyia."

1. Siku ya Sabato (Walawi 23:2-3; Mwanzo 2:1-3.)

Mungu aliendelea kusema, "Mbele ya kueleza juu ya karamu, Musa ukumbushe watu kwamba siku ya saba ya kila juma ni Sabato - siku ya kupumzika."

Mungu aliweka siku ya saba kama siku ya kupumzika wakati gani? (Uwakumbushe juu ya Mwanzo 2:1-3) Alitolea Waisraeli mufano kwa "kupumzika" siku ya saba nyuma ya siku sita ya kuumba.

Nyuma ya Mungu aliwapa Waisraeli amri kumi. Alikumbusha watu wake ya kuwa siku ya saba ilikuwa Sabato ya Mungu Bwana (Kutoka 20:9-11). Mungu alijua kwamba itakuwa rahisi kwa watu wake kusahau neno hili. Hizi aliagiza Musa tena, "Sema na watu wangu kwamba ni lazima wasifanye kasi Siku ya Sabato. Lakini watapumuzika. Watakumbuka maajabu niliyofanya kuwaokoa toka utumwa wa Misri." (Ona Kumbukumbu la Torati 5:12-15)

Onyesha taswira 1: Kwanza haikuwa ngumu kwa watu kutii amri hii. Hawakufanya kazi siku ya Sabato. Baba walikutanisha jamaa zao kuwakumbusha maajabu MUngu aliyofanya. (Uwakumbushe Kutoka 7-12)

Lakini wakati miaka ilipopita, watu walisahau. Walianza kufanya kazi siku ya Sabato. (Ona Nehemia 13:15-18). Waliweza kuasi hivi namna gani?

Ngoja kwanza. Mbele ya kushitaki Waisraeli, ujiulize ulizo. Unatoa siku moja kwa Mungu kupumzika na kuabudu? Ao unatumia kila siku kutumika na kucheza?

Bwana Yesu alifufuka toka wafu siku ya yenga, siku ya kwanza ya juma. Tangu siku ile, siku ya kwanza ya juma ilipata kuwa siku kwa Wakristo kuabudu. (Ona Luka 24:1-7; Waebrania 10:25). Unaheshimu Bwana siku hii?

2. Siku ya Pasaka (Walawi 23:4-5; Kutoka 12:1-51; Torati 16:1-8.)

Zaidi ya kuweka Sabato kwa Mungu, sharti Waisraeli kuangalia siku takatifu fulani. Kwa njia ya Musa, Mungu alitoa maelezo kwa watu wake. "Kila mwaka kwa mwezi wa ine, ninataka mukumbuke usiku ule wana wenu wakubwa walichungwa kwa Misri. Hii itakuwa Karamu ya Pasaka. Wakati Malaika ya Mauti alipoona damu juu ya kila mulango, alipita juu ya watu wangu. Lakini wana wa Wamisri waliuawa."

Onyesha taswira 2: Mungu aliongeza kusema, "Ni hivi ninataka watu wangu kukumbuka usiku huu. Mara moja kila mwaka kila jamaa ataua kondoo dume mukamilifu kama Waisraeli walivyofanya usiku ule kwa Misri. Watoto wenu watauliza, 'Tunafanya hili kwa nini?' Baba wataeleza hivi: Baba wataeleza hivi: 'Mungu aliokoa wana wetu wazaliwa wa kwanza wote wakati malaika ya mauti alipopita kwa Misri. Wale ambao walimutii kwa kunyunyiza damu kando kando ya milango yao, walikaa salama."

Mwaka kwa mwaka Waisraeli walitii kushika Karamu ya Pasaka kama Mungu alivyoagiza. Elfu za wana-kondoo waliuawa. Kisha siku moja, karibu na miaka 1,500 nyuma ya wakati Mungu alipotoa maagizo haya, maneno yaligeuka. Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alitolewa kwa zambi zote za ulimwengu wote. (Ona Luka 23:33, 46; 1 Wakorinto 5; 7; 1 Petro 1:18-19). Tangu wakati ule, hawahitaji kutoa kondoo ao nyama wengine. (Ona Waebrania 10:10-14). Wala hakuna sababu sasa kushika Karamu ya pasaka. Kwa sababu Kristo,

Mwana-Kondoo mukamilifu akimwanga damu yake mwenyewe, wale ambao wanamwamini wataepuka mauti ya milele. Kama wewe ni wake, unamushukuru kwa neno hili? Maisha yako inaonyesha shukrani yako?

3. Karamu ya Mukate Usiotiwa Chachu (Walawi 23:6-8; Kutoka 12:14-20.)

Nyuma ya kunyunyiza damu ya mwana-kondoo kando kando ya milango, Waisraeli waliingia nyumba zao. Kila jamaa walipika na kula mwana-kondoo aliyechinjwa kuponyesha mwana wa kwanza. Walikula chakula cha mwisho kwa Misri - walikula mwana-kondoo na Mukate usiotiwa chachu. (Mwalimu: Uelezee wanafunzi wako kwamba chachu inatiwa ndani ya unga ya mukate ili mukate uweze kufufuka. Mukate pasipo chachu ni pana).

Katikati ya usiku, wana wa Wamisri walikufa na jamaa zao waliogopa sana. Wakasihi watu wa Mungu kuacha inchi yao mara moja. Waisraeli wakakamata vitu vyao mara moja wakakwenda kwa haraka kwa Bahari Nyekundu.

Mungu alikumbusha Musa: "Usiku ule ulikuwa mwanzo wa maisha yenu mapya chini ya uongozi wangu, usiache watoto wenu kuusahau. Kuwasaidia kukumbuka, sharti mufanye Karamu ya Mukate Usiotiwa chachu kila mwaka katikati ya mwezi wa ine." Musa alisikiliza kwa angalifu. Mungu alieleza namna watu watakavyofanya wakati huu mutakatifu wa juma moja:

(1) "Musifanye kazi yo yote ila kutengeneza chakula kwa jamaa zenu siku ya kwanza na siku ya mwisho wa karamu hii takatifu.

(2) "Kwa siku mbili sharti watu wote wakutane kwa ibada ya shukrani na furaha.

(3) "Sharti kila jamaa wanitolee zabihu kila siku kwa siku saba za karamu.

(4) "Mukate usiotiwa chachu tu unaweza kuliwa wakati wa juma nzima. Watu hawawezi hata kuwa na chachu nyumbani mwao juma lile. Mutu yeyote anayeasi amri hii na kula mukate uliotiwa chachu wakati wa juma hili, sharti awekwe inje ya kambi. Hawezi kuwa na ushirika na watu wangu."(Ona Kutoka 12:19).

Unajiuliza kwa nini Mungu aliona kula mukate usiotiwa chachu kuwa neno kubwa? Katika Biblia, chachu ni ukumbusho wa uovu kwa sababu inachachisha ao kuharibisha vitu. (Ona Matayo 16:11-12; 1 Wakorinto 5:7). Mukate unaotiwa chachu si mwovu. Lakini ulikuwa mafundisho kukumbusha Israeli kwamba namna chachu inavyochachicha, vivyo hivyo zambi inaharibu ushirika na Mungu. Sharti zambi iondolewe toka maisha yao kama walikuwa wakitaka kupendeza Baba yao aliye mbinguni.

Leo hatufanyi Karamu ya Mukate Usiotiwa chachu. Lakini Mungu anakumbusha Wkristo na mafundisho namna yake. (Soma 1 Wakorinto 5:7-8). Zambi ni maovu. Zambi inatuzuiza tusitii Mungu.

Onyesha taswira 3: Hivi anatuagiza kuondosha zambi toka maisha yetu, (Ona 2 Wakorinto 7:1) kama waisraeli walivyoondosha chachu zote toka nyumba zao. Anataka maisha yetu kuwa pasipo uovu kama mukate pasipo chachu. (Kitu kiviringo katika mfano kinatukumbusha mukate usiotiwa chachu na usiofufuka).

Mungu anataka tusome Neno lake, tulijifunze na kwaza juu yake. (Ona Zaburi 119:9, 11, 18, 27, 105, 130). Kwa njia ya kufanya hivi, tutakuwa Wakristo wanaopendeza Bwana Mungu.

4. Karamu ya matunda ya kwanza (Malimbuko) (Walawi 23:9-14; 1 Wakorinto 15:20-23.)

Siku nyingine takatifu iliyoshikwa ka mwezi wa ine vilevile ilikuwa Malimbuko (Matunda ya kwanza). Ile haikuwa ukumbusho wa maneno yaliyotokea zamani. Ilikuwa picha ya tokeo litakalokuwa nyuma. Sisi tunaweza kuifahamu vema kuliko Waisraeli kwa sababu ilikuwa picha ya Mutu atakayefika nyuma.

Watu wa Israeli hawakupanda mashamba wakati walipotembea jangwani. Hivi hawakuvuna mavuno. Walipata chakula namna gani? (Ukumbushe madaraka ya Mungu ya mana na kanga katika Kutoka 16)

Akiangalia saa wakati watu wake watakapoacha mazunguko yao jangwani na kuwa katika inchi ambayo aliwaahidi, Mungu alitoa maelezo kwa Musa, akisema, "Wakati munapofikia inchi pahali ninapowaongoza ninyi, mupande mashamba. Nitawapa ninyi jua na mvua. Mbegu zenu zitaota na mutavuna mavuno mazuri. Wakati nafaka zinapoanza kukomea, kwendeni shambani siku ya kwanza ya juma (siku nyuma ya Sabato).

Onyesha taswira 4: (Funika sehemu ya juu ya taswira)**:** Mungu akendelea kusema, "Kata furushi la nafaka na kulipeleka kwa kuhani. NI toleo la shukrani kwangu mbele ya kula nafaka ninyi wenyewe."

Hizi zilikuwa malimbuko ya mavuno. Ni kwa sababu hii siku hii takatifu iliitwa Karamu ya Malimbuko… Nafaka na matunda mengi yatakuwa kwa watu, lakini nafaka ya kwanza itakuwa kwa Mungu.

Sasa tuone nini Mungu anafundisha juu ya malimbuko. (Mwalimu: Sema na watoto kusoma 1 Wakorinto 15:20-23 pamoja nawe. Kama wasipoweza kufanya hivi, soma mashairi haya polepole mara chache.)

Nani anaitwa malimbuko katika mashairi haya? (Kristo). Miaka 1500 nyuma ya Mungu kusema juu ya Malimbuko, Kristo alikufa. Yeye, Mwana-Kondoo wa Pasaka, hakubaki juu ya musalaba, wala hakubaki kaburini.

Siku ya Bwana, siku ya kwanza ya juma - siku nyuma ya Sabato - alifufuka toka wafu! (Onyesha sehemu ya juu ya taswira 4). Alikuwa wa kwanza kufufuka toka wafu na kuwa na mwili wa ufufuko. Ni kwa sababu hii anaitwa malimbuko.

Kwa sababu Kristo alifufuka, kila mutu ambaye anamwamini kuwa Mwokozi atafufuka vilevile. Wakati gani? Wakati Kristo atakapokuja katika hewa kupeleka waamini wote mbinguni. (Ona 1 Wakrointo 15:23; 1 Watesalonika 4:13-18). Hili ni tumaini bora kuliko yote ambayo mutu yeyote anaweza kuwa nayo. Una tumaini hili? Unamungojea kuja katika hewa?

Mungu alitaka Waisraeli kukumbuka maneno yote ambayo aliwafanyia. Na anataka ukumbuke maneno yote ambayo alikufanyia. Unaheshimu Bwana siku yake? Unaishi maisha inayoonyesha shukrani yako kwa Mwana-Kondoo wa Mungu? Unajitenga na chcahu ya zambi, ukijaribu kusihi maisha safi na takatifu? Unangoja kuja kwa Bwana Yesu katika hewa?

Kama ukihitaji kusema “hapana” kwa maulizo haya mengine, utasema na Mungu juu yake sasa hivi?

SOMO 2 - KARAMU ZA BWANA (Sehemu ya pili)

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Walawi 23:15-44

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba karamu takatifu zilionyesha matukio yaliyopita na vile yale yatakayokuja.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kama Neno la Mungu ni kweli na kila kitu kinaahadiwa ndani yake hakika kitafanyika.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Furaha kwa sababu Mungu anakuwa na mipango zenye enzi kwa watu wake.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kujitayarisha kwa kurudi kwa Krsito. Kuombea Wayuda kusudi wageuke kwa Yesu, Masiya wao.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)

1. Karamu ya Pentekote (Walawi 23:15-22; Matendo 2:1-47.)
2. Karamu ya Baragumu (Walawi 23:23-25; 1 Watesalonika 4:13-18.)
3. Siku ya Upatanisho (Walawi 23:26-29.)
4. Karamu ya Vibanda (Walawi 23-33-44.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mimi ni Bwana Mungu wenu… Mutashika amri zangu zote, na hukumu zangu zote; na kuzitenda: Mimi ni Bwana." Walawi 19:36b-37

Maelezo kwa mwalimu:

Mungu anajua kwamba ni nyepesi kwa watu kumusahau. Hivi alionya Israeli juu yake. (Ona Torati 6:12-13). Aliwatolea karamu saba kila mwaka kuwakumbusha juu ya utunzi wake. Wakati unapofundisha kumbuka makusudi mawili ya karamu: (1) Zilikumbusha Waisraeli siku zote juu ya Mungu - Yeye ni nani na maneno ambayo aliwafanyia; (2) Ni kwa wao mifano mitakatifu ya kusudi la Mungu kwa wakati wa kuja.

Kama ukiona ni kugumu kwa watoto kufuata mafundisho yote ndani ya somo moja uligawe kwa masomo mawili ao matatu. Ukumbushe wanafunzi tena na tena wakati unapoendelea na mafundisho ya karamu.

Somo: Unakumbuka nini ulifanya mwaka wa mbele kwa tarehe hii? (Taja tarehe ya leo). Unaweza kukumbuka jambo uliyofanya mwezi uliopita kwa tarehe hii? Yanatusahau mbiombio!

Kwa nini Mungu aliagiza Israeli kufanya Karamu takatifu saba kila mwaka? (Usaidie wanafunzi kujibu). Waisraeli hawakuwa na Biblia kama sisi. Hivi hawakufahamu kwamba karamu zao takatifu saba zilionyeha picha ya matokeo watakayokuja katika shauri la Mungu. Kwa sababu tuna Biblia nzima leo, tunajua matukio haya. (Wakati unapowakumbusha juu ya karamu tatu za kwanza, uonyeshe picha za somo la kwanza. Sema nao juu ya historia ya karamu na ya kwamba ni mifano ya matokeo yatakayokuja.)

(1) Pasaka - mufano wa Kristo Yesu, Mwana-Kondoo wa Pasaka atakayekufa kutukomboa - kutupatia sisi uhuru toka zambi.

(2) Karamu ya Mukate Usiotiwa chachu - Ukumbusho ya kuwa zambi inaharibu ushirika wa mwamini na Mungu. Sharti watoto wa MUngu wasome Biblia kukua katika imani wawe Wakristo wa nguvu, wakikiri zambi zinazozuiza ushirika wao na Mungu, Yule aliye Mutakatifu.

(3) Karamu ya Malimbuko - Picha ya ufufuko wa Kristo toka wafu. Ufufuko wake unahakikisha kwamba sisi tutafufuka vilevile kutoka wafu.

Waisraeli walingoja siku za karamu takatifu na furaha. Hawakufanya kazi siku zile. Lakini hawakuweza kufanya mapezi yao. Mungu alieleza waziwazi watakayofanya kwa kila siku.

Musa aliagiza kwa uangalifu kwa maelezo ya Mungu. Nyuma atasema na viongozi wa Israeli nini Mungu aliagiza.

1. Karamu ya Pentekote (Walawi 23:15-22; Matendo 2:1-47.)

Mungu alianza kusema: “Musa, hesabu siku 50 kutoka siku ile ulifanya Karamu ya Malimbuko. Hii itakuwa siku takatifu itakayofuata Karamu ya malimbuko. Ni Karamu ya Pentekote.”

Unakumbuka wakati Karamu ya malimbuko ilipokuwa? (Katikati ya mwezi wa ine). Hivi Karamu ya Pentekote itakuwa siku gani? (Usaidie wanafunzi kuhesabu ya kuwa itakuwa mwezi wa sita).

Mungu aliendelea kusema: “Musa, Karamu ya Pentekote itakuwa kwa wakati wa kuvuna ngano. Kila jamaa atapoka mikate miwili ya unga ya ngano. Watapeleka ile kwa Hema na kuitoa kuwa shukrani kwa baraka zangu. (Ona Torati 16:10). Pamoja na mikate, mulete zabihu za nyama.”

Kwa nini ni lazima watoe zabihu za nyama wakati walipoabudu Mungu? (Pasipo kumwanga damu wenye zambi hawakuweza kupokelewa na Mungu Mutakatifu. (Ona Walawi 4:20; 17:11; Waebrania 9:22)

Mungu aliongeza akisema: “Hakuna mutu anayeweza kutumika kazi kwa siku hii takatifu. Sharti kila mutu afanye karamu ya Pentekote na furaha kubwa. Watoto watawauliza ninyi kwa nini munafurahi sana. Muwaambie: ‘Tulikuwa watumwa kwa Misri, lakini Mungu alitupatia sisi uhuru ili tuweze kutii sheria zake.’” (Ona Torati 16:12)

Waisraeli walichunga siku hii takatifu kwa uangalifu wakati walipokuwa jangwani. Nyuma, walikaa inchini Mungu aliyowapa wao. Wakati ule, wanaume walikwenda Yerusalema kila mwaka kwa Karamu ya Pentekote. (Ona Matendo 2:1; sawanisha na 20:6). Walifanya hivi kwa mia za miaka. Mwaka Kristo alipokufa, akafufuka, na kupanda mbinguni, elfu za watu walikuwa kwa Yerusalema kwa Pentekote. Wayuda hawa walitoka inchi nyingi. Hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Walikataa kumupokea, yula mabaye Mungu aliahidi kutuma. Walikuwa hekaluni wakitoa mikate yao iliyopikwa na ngano zilizovunwa sasa. Walikuwa wakitoa zabihu za nyama vilevile - kama Musa alivyofundisha wtu wao mia za miaka mbele.

Lakini wanafunzi wa Kristo hawakuwa kwa hekalu. Walikuwa nyumbani. Mbele ya kurudi mbinguni, Bwana aliwatolea amri. Alisema, “Rudieni Yerusalema, mungojee Musaidizi, Roho Mutakatifu, nitakayetuma. Atawatia ninyi uhodari na uwezo kusema na wengine juu yangu. (Ona Matendo 1:8; sawanisha na Yoane 14:16-17, 26; 16:7-15; Waroma 8:26)

Onyesha taswira 5: Hivi, siku ya Pentekote, wanafunzi walikuwa wakitii amri ya Bwana. Walikuwa wakingoja kuja kwa Roho Mutakatifu. Gafla Roho Mutakatifu alishuka kukaa ndani ya wale waliaomini Yesu. (Ona Yoane 14:17). Zilikuwa siku 50 nyuma ya ufufuko wa Bwana Yesu kutoka wafu! Kuja kwa Roho kulitangazwa na uvumi, kama upepo. Ndimi zilizoonekana kama moto ziligawanyika na kukaa juu ya kichwa cha kila mutu. Kila mumoja alipata uwezo, kama Kristo alivyoahidi. Waliweza kusema lugha wasizojifunza. (Kufundisha maneno yote, tumia mwisho wa somo 2, Kitabu 14, Agano Jipya).

Tangu siku ile Roho Mutakatifu anakuja kukaa mioyoni mwa waamini wa kweli saa ile ile wanaamini Bwana Yesu Kristo. Kwa sababu Yeye ni Roho Mutakatifu wa Mungu anaweza kuwa pahali pote kwa mara moja.

Anafanya waamini kuwa jamaa kubwa moja - jamaa ya Mungu. Jamaa ya Mungu wanajulikana kama kanisa. Kanisa ni wale waliozaliwa mara ya pili walio na Roho Mutakatifu akikaa ndani yao. Waamini wanaweza kuwa Wayuda ao Mataifa. (Mataifa ni wale wasiokuwa Wayuda).

Munaona kwa nini Karamu ya Pentekote ilifanywa na mikate miwli iliyofanywa na chachu? Kanisa la Kristo lililoanzwa kwa Pentekote lina namna mbili ya watu - Wayda na Mataifa. Hata kama waliokolewa toka zambi yao na Bwana Yesu Kristo, wao si pasipo zambi. (Ona 1 Yoane 1:8). Mikate ya chachu ni ukumbusho ya kuwa waamini watakuwa na tabia ya zambi siku zote wakati wangali hapa duniani. Lakini wanakuwa na Roho Mutakatifu ndani yao vilevile. Na kama wakimupa njia kufanya hivi, atawaongoza kufanya maneno yanayopendeza Mungu.

Kuja kwa Roho Mutakatifu kulikuwa Pentekote kubwa Mungu aliyongoja kwa miaka 1500.

2. Karamu ya Baragumu (Walawi 23:23-25; 1 Watesalonika 4:13-18.)

Wakati wa Musa, Mungu aliweka siku nyingine za ukumbusho. Miezi ya saba, minane na tisa ilipita pasipo siku za karamu. Lakini katika mweziwa kumi kulikuwa karamu takatifu tatu. Mwezi wa kumi ulianza na Karamu ya Baragumu. Hii ilikuwa “Bonne Année” ya watu wa Yuda. (Mwalimu: kama watu wako wanakumbuka “Bonne Année”, zungumuza juu ya namna wanavyoikumbuka).

Hii ilikuwa siku ya furaha kwa Waisraeli. Baragumu zilipigwa. Hakuna mutu aliyefanya kazi. Wayuda hawa waliabudu Mungu na kutoa zabihu. Nyuma walikula na kushukuru Mungu kwa mema yake kwao. (Ona Nehemia 8:2, 9-12.)

Baragumu mbili zilipigwa. (Mwalimu: Ujifunze kwa uangalifu maagizo juu ya baragumu yanayoonyeshwa katika Hesabu 10:1-10. Baragumu za feza mbili zitapigwa kwa sababu mbalimbali. Katikati ya sababu hivi, mbili ni kubwa: (1) Kuita makutano; (2) Kutangaza kwamba Waisraeli wafunge vitu vyao kwa kusafiri. Kila mara baragumu zilipopigwa ilikuwa ukumbusho wa kitu kilichotokea wakati Waisraeli walipokuwa jangwani. Kwa sauti ya baragumu moja, watu waliitwa kukutana kwa makutano. Sauti ya baragumu nyingine ilikuwa kuwakutanisha kuendelea na safari yao kwenda inchi ambayo Mungu aliwapatia.

Karamu ya Baragumu inaonyesha matukio mawili yasiyotokea bado, lakini yatatokea hakika!

Onyesha taswira 6: (1) Siku moja, inaweza kuwa bado kidogo, baragumu ya Mungu itapigwa. Siku ile Bwana Yesu atashuka toka mbingu katika mawingu. Wale walio wake na wamekwisha kufa, watafufuliwa. Watakusanyishwa pamoja na waamini wote walio kwanza hai duniani. Na wote pamoja watachukuliwa kukutana na Bwana katika ewa. Makutano ya furaha kubwa! (Onyesha mushale kwa kushoto ya picha.) Kutoka wakati ule waamini wote watakuwa pamoja na Bwana. (Ona 1 Wakorinto 15:51-53; 1 Watesalonika 4:16-17).

Utakuwa pamoja na wale watakaokutana na Bwana hewani? Unaweza kujua kabisa kama umekwisha kuamini Kristo kuwa Mwokozi wako?

(2) Miaka saba nyuma, baragumu ya Mungu itapigwa tena, na Bwana Yesu atashuka mara moja duniani. (Onyesha mushale kwa kuume upande wa chini ya picha). Mara hii sauti ya baragumu ya Mungu itaita Waisraeli kusafiri kutoka dunia yote kwenda Israeli, inchi yao wenyewe. (Soma Matayo 24:29-31; sawanisha na Isaya 18:3; 27:13; Yoeli 2:1-3:21)

Karamu ya Baragumu ilikuwa wakati wa furaha. Itakuwa wakati wa furaha kubwa kwa Waisraeli wakati watakapokuwa kwa mwisho katika inchi yao.

3. Siku ya Upatanisho (Walawi 23:26-29.)

Mara moja nyuma ya Karamu ya Baragumu ilikuwa siku ya Upatanisho. (Mwalimu: Fundisha sehemu hii kwa kukagua somo 4 la Kitabu 11). Hii ilikuwa karamu ya pekee wakati watu walipokuwa na huzuni. Walikuwa na huzuni kwa sababu gani? (Walikuwa na huzuni kwa zambi zao ambazo zilizowatenga na Mungu).

Walipokea usamehe wa zambi namna gani? (Damu ya zabihu ya zambi ilifunika zambi zao.) Nani alitoa zabihu Siku ya Uatanisho? (Kuhani Mukubwa). Kuhani mukubwa alikuwa na heshima kubwa gani Siku ya Upatanisho? (Siku hii tu katika mwaka muzima, aliweza kuingia Pahali Patakatifu Sana katika Hema. Hapa Mungu alikaa juu ya Kiti cha Rehema).

Kwa nini Kuhani Mukubwa alitumia mbuzi wawili kwa zabihu ya zambi kwa siku hii? (Mbuzi mumoja alichinjwa. Kuhani Mukubwa alinyunyiza damu yake juu na mbele ya Kiti cha rehema katika Pahali Patakatifu Patakatifu. Wakati Mungu alipoona damu, alisamehe zambi za taifa nzima. Mbuzi wa pili alichukua zambi za taifa jangwani na kupotea kule. Kama mbuzi alivyopotea na kusahauliwa, vivi hivi Mungu alisahau zambi za watu. (Ona Walawi 16:1-34).

Inafaa tukumbuke Siku ya Upatanisho leo? Kwa nini? (Mbele ya kufa kwa Kristo, hata mia za zabihu zilitolewa, zilifunika tu zambi za watu kwa wakati tu. Zabihu nyingine zilihitajika. Lakini damu ya Kristo inasafisha kwa milele zambi za wote ambao wanamwamini).

Leo Wayuda wengi hawaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Hawaamini ya kuwa alimwanga damu yake musalabani kulipa azabu ya zambi.

Onyesha taswira 7: Siku inakuja wakati Bwana Yesu atakapokuja kutawala dunia. Kisha wakati anapotawala katika uwezo na utukufu, Wayuda wengi watatubu. (Ona Matayo 24:30). Kwa siku ile itakayokuja kama kwa Siku ya Upatanisho, watakuwa na huzuni na kuomboleza. Kwa nini? Kwa sababu walikataa Kristo. (Ona Zekaria 12:1-14). Kwa wakati ule, wengi watageuka kwake, wakiamini ya kuwa kweli yeye ni Mwana wa Mungu, Mwokozi wao. Na Mungu anaahidi kwamba Waisraeli wengi wataokolewa kwa wakati ule. (Ona Waroma 11:26; Yeremia 31:34; Waebrania 8:12; 10:16-17).

4. Karamu ya Vibanda (Walawi 23-33-44.)

Siku tano nyuma ya Siku ya Upatanisho, kulikuwa siku takatifu nyingine. Hii ilikuwa Karamu ya Vibanda. Iliendelea kwa siku saba.

Wakati Waisraeli walipotembea jangwani miaka makumi ine, walikaa katika hema. Waliongozwa na Mungu toka pahali pamoja hata pahali pengine. Walifunga hema zao na kuzisimamisha tena mara nyingi. Mungu alitaka wakumbuke safari zao wakati walipofika inchi ya ahadi na kukaa katika nyumba.

Hivi katikati ya mwezi wa kumi, kila jamaa watakata matawi na kufanya kao. Kisha jamaa yaote walichama kwa kao kwa siku saba. Ninazani ilikuwa furaha kubwa kwa watoto! Ilikuwa sawasawa na kwenda kwa kambi. Wengi waliuliza baba zao: “Kwa nini tunafanya neno hili?”

“Mungu anataka tukumbuke alivyoongoza watu wetu toka Misri. Anataka tukumbuke namna tulivyokaa ndani ya hema na namna alivyotulinda jangwani.”

(Mwalimu: Kagua kidogo namna Mungu alivyotolea maji na chakula kwa Waisraeli. Kutoka 15:1-27; 16:1-36; 17:1-7. Vile namna alkivyowalinda wasishindwe na Amaleki, Kutoka 17:8-16. Ona Kitabu 8, Agano la Kale masomo 1, 2, 3)

Karamu ya Vibanda ilikuwa wakati mutakatifu wa furaha kubwa kwa watu wote. Wao wote walikumbuka mema ya Mungu kwao.

Lakini wakati wa furaha kubwa kupita unakuja kwa watu wa Mungu, ndio Wayuda. Tulijifunza kwamba Bwana Yesu atakuja duniani tena. Baragumu ya Mungu itaita Waisraeli kurudia Yerusalema. Wakati watakaoona Kristo, wengi kwa mwisho wataamini kwamba yeye ni Masiya yao, Mwana wa Mungu.

Onyesha taswira 8: Kisha Bwana Yesu atakuwa mutawala juu ya dunia yote kwa miaka 1000. (Ona Ufunuo 20:4, 6). Utakuwa wakati wa furaha kabisa kwa wayuda wanaoishi wakati ule!

Leo kuna Wayuda wengi wasiosikia Habari Njema bado. Andika majina ya Wayuda ambao unawajua. Kisha tuombe Mungu kukupa nafasi kuwaambia juu ya Bwana Yesu juma hili.

Mungu ana shauri nzuri sana kwa wakati wa kuja kwa watu wake wote. Kama wewe si mutoto wake, lakini utamugeukia leo, wewe vilevile unaweza kuwa ndani ya shauri lake kwa wakati wa kuja. Utamwamini sasa hivi? (Mwalimu: Funga somo lako na kuomba watoto waje kwako na kuomba. Halafu uombe wanafunzi wako kufika mara ya nyuma na kitu walichofanya kwa wao wenyewe.)

SOMO 3 - PUMZIKO NA UHURU

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Walawi 25; mashairi yaliyo katika somo.

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba sheria za Mungu kuongoza waisraeli zilikuwa kwa baraka yao.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwani Mungu aliyeumba Waisraeli, anakuwa na ruhusa kuwatawala pamoja na inchi yao.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Ukumbusho wa uhaki wa Mungu juu ya maisha yao na hamu ya kutii amri yake.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kutii mapenzi na amri za Mungu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Pumziko kwa inchi (Walawi 25:1-7, 19-23.)
2. Uhuru kwa watu (Walawi 25:8-18, 39-55.)
3. Azabu ya Mungu kwa wenye kuasi (Walawi 26.)
4. Uhuru wetu na upumziko (Yoane 8:32-36; Waebrania 4:1-10.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mimi ni Bwana Mungu wenu… Mutashika amri zangu zote, na hukumu zangu zote; na kuzitenda: Mimi ni Bwana." Walawi 19:36b-37

Maelezo kwa mwalimu:

Mbele ya kufundisha somo hili, ukumbushe wanafunzi somo kwa uangalifu. Inajaa na mafundisho makubwa juu ya wakati wa kupita na wakati wa kuja kwa Waisraeli. Haiwezekani kufahamu Neno la Mungu vizuri pasipo kujua wazi shauri la Mungu kwa Waisraeli. Ukumbushe wanafunzi maneno haya tena na tena.

Somo: Ulileta nini kwa darasa leo ambacho ulijifanyia? (Acha wanafunzi kuonyesha vitu walivyoleta na kusema juu yao. Onyesha kitu ulichofanya vile. Uonyeshe ya kuwa kwa sababu walivifanya I vitu vyao. Hivi wanaweza kufanya kama wanavyotaka navyo. Kama wakiacha mutu mwengine kuvitumia, wanaweza kumwambia namna gani kuvichunga).

Nani alifanya dunia? (Ona Mwanzo 1:1). Hivi dunia ni ya nani? (Zaburi 24:1; 1 Wakorinto 10:26) Maana yake ni kwamba Mungu anaweza kufanya kama anavyotaka na dunia? (Zungumuza).

Mia za miaka za mbele, Mungu aliongoza Abrahamu kufika kwa Kanana. (Mara nyingi inaitwa Palestina na sasa inaitwa Israeli). Pale Mungu alitoa ahadi hii: "Abrahamu ninakupa wewe inchi hii kwa watu wako watakaozaliwa nyuma yako, itakuwa inchi yenu milele" (Ona Mwanzo 7:8)

Mungu hakugeuza kamwe ahadi hii. Watu wengi kutoka inchi nyingine walikaa kwa Palestine. Lakini ni mali ya Wayuda (Wazao wa Abrahamu). Kwa macho ya Mungu itakuwa yao siku zote, hata kama adui wanakaa pale kwa wakati. Mungu hakutoa sehemu nyingine ya dunia kwa taifa fulani. Lakini kumbuka, Israeli ni taifa chaguliwa la Mungu.

Mungu alitumia wakati wa njaa kuongoza Yakobo (mujukuu wa Abrahamu) na jamaa yake kutoka Kanana kwenda Misri. Walikaa pale miaka 400. Kisha Mungu aliwaongoza kurudia inchi yao tena.

Alisema na Musa aliyekuwa wa jamaa ya Yakobo (muzao). Mungu alisema, "Musa inchi ya Kanana (Palestine) ni yangu. Nimechagua kuitole watu wangu, Israeli.. Nina sheria ambazo inapasa Waisraeli watii katika inchi hii. Sheria hizi ni kwa baraka yao wenyewe. Angalia kabisa kwamba wanafahamu sheria zangu." (Ona Walawi 25:23)

1. Pumziko kwa inchi (Walawi 25:1-7, 19-23.)

Musa alikutanisha viongozi wa Israeli. Makutano yao yaliweza kuwa hivi: "Wanaume, munajua Mungu anatuongoza kurudia inchi ya baba zetu - Abrahamu, Isaka na Yakobo."

Wanaume wote waliinamisha vichwa vyao kukubali. Musa aliendelea kusema: “Wakati tunapofika pale, kila jamaa watapokea sehemu ya udongo kukaa juu yake na kulima. Mungu alisema kwamba mutapanda mbegu na kuvuna nafaka kwa miaka sita. Kisha mwaka wa saba sharti mupumzishe udongo. Sharti musipande kitu.”

Wanaume walisema: “Tutakula nini kama tusipopanda kitu mwaka ule?”

Musa alieleza: “Musifazaike. Mungu anaahidi kuwatolea ninyi mavuno makubwa mwaka wa sita. Kweli, mavuno ya mwaka ule yatatosha hata kwa miaka mitatu! Mwaka wa sita mavuno yatapita mahitaji ya mwaka ule. Kutakuwa mengi kwa mwaka wa saba wakati musipopanda mashamba na yatatosha kwa mwaka wa nane hata kufika wakati munapovuna tena.” (Ona Walawi 25:21).

Mutu mumoja aliuliza: “Tutafanya nini namatunda yanayoota juu ya mizabibu na miti wakati wa mwaka wa saba?”

Musa alijibu: “Mutu yeyote anaweza kuyakula, hata ni juu ya udongo ya wanani.”

Mwengine aliuliza: “Kama tusipotumika shambani mwetu tutafanya nini na saa yetu?”

Onyesha taswira 9: Musa alijibu: “Mutakuwa na saa kupita kufundisha watoto wenu sheria za Mungu. Kisha, wao vilevile watamutii.” (Ona Torati 31:10-13)

Kila mwaka wa saba, Mungu alitaka kutolea israeli mahitaji yao bila kutumika kazi. Iliwapasa kumwamini tu kuwalinda na kumutii.

2. Uhuru kwa watu (Walawi 25:8-18, 39-55.)

Musa akaendelea kueleza sheria za Mungu kwa viongozi wa Israeli.

“Wakati munapokaa katika inchi ya Kanana, mwaka wa makumi tano utakuwa mwaka muhimu kwa ninyi.”

Mutu moja aliuliza: “Maana ya mwaka wa makumi tano ule ni nini?

Musa alisema: “Kila mwaka wa makumi tano utakuwa mwaka wa Yubile… Siku ya Upatanisho, mwaka ule, baragumu italia kutangaza mwaka muzima wa uhuru na furaha kubwa kwa watu wote.”

Mwengine aliuliza: “Mwaka wa Yubile utakuwa mbali na mwaka mwengine kwa njia gani?

Musa alieleza kwa uangalifu:

(1) “Kwanza, hamutapanda mashamba yenu. Mungu atawatolea ninyi vyakula vingi kama atakapofanya kila mwaka wa saba.”

Mutu mumoja akisimama, akasema: “Maana yake ni ya kuwa hatutapanda mashamba kwa miaka miwili. Mwaka wa makumi ine na tisa utakuwa mumoja wa miaka saba wakati tunapopumzisha udongo wetu. Na mwaka wa makumi tano utakuwa mwaka wa Yubile. Tutakulisha jamaa zetu namna gani?”

Musa alijibu: “Mungu meahidi kuwapa ninyi mavuno makubwa wakati wa miaka makumi manane. Hivi mutakuwa na vyakula vya kutishag. Anataka mumwamini. Anataka muamini kwamba atachunga ahadi yake.”

(2) Musa alisema tena: “Wakati wa miaka makumi na tisa mbele ya Yubile, labda jamaa wengine watahitaji feza. Wanaweza kuuzisha udongo ao nyumba zao kuipata. Katika mwaka wa Yubile, vitu walivyouzisha vitarudishwa kwao.”

(3) Musa alitangaza tena: “Lakini neno kubwa kupita, uhuru kwa watu wote utatangazwa katika mwaka wa Yubile.”

Viongozi waliuliza: “Uhuru? Kwa nini ni lazima uhuru utangazwe kwa watu wote? Tuna uhuru! Sisi hatuko watumwa! Sisi ni huru!”

Musa aliwakumbusha: “Ndiyo, ndiyo! Ninyi ni huru, lakini kutakuwa watu watakaokuwa na deni wasiloweza kulipa. Wakati neno hili linapotukia, wanaweza kwenda kwa mutu ambaye wana deni kwakena kusema: ‘Sina mali kulipa deni langu. Nitakuwa mutumishi wako. Nitakutumikia hata deni langu linapokwisha kulipwa!’

“Mara nyingine watu watakuwa masikini hata hawatakuwa na vyakula vya kutosha. Watakwenda kwa mutu tajiri na kusema, ‘Nitakuwa mutumishi wako kama utanipa mimi na jamaa yangu pahali pa kukaa, vyakula kula, na mavazi ya kuvaa.’

“Kutoka siku ile mutu yule hatakuwa na uhuru. Atakuwa mutumishi na kutumika nguvu kwa bwana yake. Atapewa mahitaji yake tu.” (2 Wafame 4:1)

Onyesha taswira 10: Musa alieleza, “lakini kwa mwaka wa yubile madeni yote yatafutwa na kusahauliwa. (Onyesha taswira ya juu) na watumishi wote watapata uhuru.” (Onyesha taswira ya chini).

Mwaka wa yubile utakuwa mwaka wa furaha kubwa. Wote wataweza kuanza tena - mwanzo mupya!

Kweli Mungu alipenda watu wake, Waisraeli. Alitaka wawe na maisha mazuri katika inchi yao wenyewe. Sheria zake zilikuwa kamilifu. Kama wangetii maagizo yake, wangekuwa na furaha nyingi.

3. Azabu ya Mungu kwa wenye kuasi (Walawi 26.)

Miaka makumi ine ilipita mbele ya Waisraeli kufika kwa inchi ambayo Mungu aliwatolea. Musa amekwisha kufa. Yosua alikuwa kiongozi wao. Aligawa inchi katika ya jamaa zote, kama Mungu alivyoamuru.

Kila jamaa walitumika nguvu kusafisha inchi yao, kulima udongo, na kupanda mbegu. Mungu alituma mvua na jua, na mbegu ziliota. Watu walifurahi sana kwa sababu ya mavuno mazuri ambayo Mungu aliwatolea!

Miaka sita ilipita. Wakati ilipokuwa saa kuacha inchi kupumzika, hakuna mutu aliyekumbuka! Waliweza kusahau nama gani wakati Mungu alipowatendea mema hivi?

Watu wa Mungu wlifanya urafiki na watu wa Kanana wasioabudu Mungu wa kweli. Watu wale hawakupumzisha inchi yao. Wayuda walisahau amri za Mungu. Wakasahau kufundisha watoto wao amri za Mungu.

Onyesha taswira 11: (Onyesha sehemu ya juu; funika sehemu ya chini).Miaka ilipita. Mungu alituma wajumbe ya kuwa kama wasipotii atawaazibu. Lakini hawakusikiliza. (2 Mambo ya Siku 36:15-16).

Mungu alikuwa na saburi kwa miaka mingi. Kisha aliacha Wababeli kushinda Waisraeli. (Onyesha sehemu ya chini ya taswira). Wababeli walipeleka Waisraeli kwa Babeli na kuwachunga kama wafungwa wa vita kwa miaka 70 (2 Mambo ya Siku 36:16, 18).

Kwa miaka ile 70 inchi iliweza kupumzika kama Mungu alivyoshauri. (Ona Walawi 26:34-35, 43; 2 Mambo ya Siku 36:21). Waisraeli walijua sasa kwamba Mungu atafanya hakika kama alivyosema. Wakafahamu kwamba kusahau Mungu ni uovu. (Yeremia 2:19). Walijifunza nyuma kabisa ya kuwa Mungu anahukumu kutokutii.

Watu walilia: “Kama tungalisikiliza Mungu! Kama tungalikumbuka sheria zake! Kama tungalimutii!”

Lakini saa imekwisha kupita. Walikuwa wafungwa wa wageni. Hawakuweza kuishi kama watu wa uhuru kama Mungu alivyokusudi.

4. Uhuru wetu na upumziko (Yoane 8:32-36; Waebrania 4:1-10.)

Tumekuwa tumezungumuza juu ya sheria Mungu alizotoa kwa Waisraeli zamani wakati walipokuwa karibu kuingia inchi ambayo Mungu aliwaahidi kuwapa. Sasa tuwaze juu ya amri nyingine Mungu anazokuwa nazo kwa sisi leo.

(1) Bwana Yesu anasema: “Mutajua kweli, na kweli itawaweka ninyi huru” (Yoane 8:32) Hii ni amri ya Mungu. (Sema tena na tena ili wanafunzi waijue kwa nia)

Labda munawaza: “Mimini huru. Mimi si mutumwa. Haifai nipate uhuru!”

Yesu anajibu: “Yule anayefanyaga zambi ni mutumwa wa zambi.” (Ona Yoane 8:34)

Nani anafanya zambi? (Usaidie mazungumuzo. Uwaambie nguvu masemo ya Waroma 3:23, na kuonyesha kwamba ni WATU WOTE waliofanya zambi: Hivi ni wewe na mimi vilevile. Hatukuchagua kuwa watumwa wa zambi. Tunazaliwa wenye zambi. (Ona Zaburi 51:5; Waroma 3:10-12).

Tunaweza kupata uhuru namna gani? “Kama Mwana anawaweka ninyi huru, mutakuwa huru kweli.” (Yoane 8:36). Nani ni Mwana? (Yesu Kristo).

Onyesha taswira 12: Sisi, wewe na mimi, tunaweza kupata uhuru kwa njia ya Yesu Kristo namna gani? Kwa njia ya kumwamini yeye aliyetoa damu yake ya damani musalabani. Tunaunuliwa kwa bei! Hakuna njia nyingine kupata uhuru.

Mungu anaahidi uzima wa milele pamoja naye mbinguni kwa wote waliowekwa huru na Yesu Kristo. Lakini anaonya ya kwamba wote wanaokataa kuamini Mwana wake kuwa Mwokozi wao watahukumiwa kwa milele katika hadeze. (Ona Yoane 3:18, 36).

Waisraeli waliasi Mungu. Walijifunza nyuma ya kwamba Mungu atafanya kama alivyosema. Utangoja vilevile hata wakati unapita? Ao utapokea Kristo leo?

(2) Mungu anatuagiza kupumzika na kumwamini (Waebrania 4:1, 10). Maana ya kupumzika na kuamini ni kutumika nguvu? Hapana! Lakini hata hivi watu wanatumika nguvu waweze kuwa wenye kufaa kuingia mbinguni! (Zungumuza juu ya vitu watu wanavyofanya kupendeza Mungu: Kwendakwa kisomo, kwenda kwa sanamu, kuwasha taa, kutoa mali, kukumbuka siku fulani, na vivi hivi).

Mungu anaona mambo wanayofanya na kusema, "… haki zenu zote ni kama vitambaa vya kuapasukapasuka vya taka!" (Isaya 64:6)

Unajarbu kuwa mwema kufaa kwenda mbinguni? Uwezi kuwa mwema kufaa kamwe! Njia moja tu ya kuwa mwema kufaa ni kuamini Bwana yesu Kristo (Matendo 16:31). Tia imani yako yote ndani yake. Kwa njia ya mauti yake na ufufuko wake alifanya yote Mungu aliyotaka. Anataka tu umwamini na kazi kubwa aliyofanya.

Hizi ni sheria za Mungu. Ni kwa baraka yetu. Alituumba. Anatupenda. Utachagua kumutii na kufurahi ndani ya baraka zake leo?

SOMO 4 - BARAKA AO AZABU

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Walawi 26; Torati 28; mashairi yaliyo katika somo.

Shabaa ya somo: Kuonyesha ya kuwa Mungu aliolea Waisraeli uchaguo utakaogeuza maisha yao.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Hata Waisraeli walikosa kwa uchaguzi wao, Mungu angali na mipango kwa watu wake.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu kubwa ya uhuru utawaruhusia kuchagua yeye watayetumikia na kumutii.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kuchagua leo kutumikia Mungu na kumutii.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Maonyo juu ya sanamu (Walawi 26:1-2.)
2. Baraka kwa kutii (Walawi 26:3-13; Torati 28:1-14.)
3. Laana ya kutokutii (Walawi 26:14-39; Torati 28:15-68.)
4. Ukosefu wa Israeli na tumaini lao kwa wakati wa kuja (Walawi 26:40-45; Yeremia 23:7-8; 30:3; 31:33-34.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mimi ni Bwana Mungu wenu… Mutashika amri zangu zote, na hukumu zangu zote; na kuzitenda: Mimi ni Bwana." Walawi 19:36b-37

Maelezo kwa mwalimu:

Zamani, Mungu aliwapa waisraeli njia kuchagua. Kama wakitii amri zake, aliahidi kuwapatia baraka nyingi za dunia. Kama wakimwasi, wataazibiwa. Walichagua kuasi. Na leo, mia za miaka nyuma, wangali wanateswa na azabu ya Mungu kwa sababu ya chaguo yao mbaya. Hata hivi, Mungu alichagua Waisraeli kuwa watu wake wa pekee. Hivi siku itakuja wakati wengi wao watakapogeuka kwa Kristo. Na Mungu atawarudisha kwa inchi yao. Kisha atawabariki kama alivyoahidi.

Sisi vile tunaweza kuchagua. Tunaweza ufanya chaguo. Lakini tunapashwa kukumbuka kwamba itatupasa sisi tunaoamini Kristo kusimama mbele ya kiti chake cha hukumu. Pale yeye Mwamuzi wa haki atahukumu kazi zetu. (Ona 2 Wakorinto 5:10). Kitu chochote tunachopanda tutavuna. (Ona Wagalatia 6:7-8). Mwalimu, chaguo zako zinapatana na mapenzi ya Mungu? kama ndivyo, maisha yako itakuwa mufano muzuri kwa wanafunzi wako. Mazungumuzo ya Finehasi na baba yake ni ya mawazo tu. Musa alipokea amri kutoka kwa Mungu na kuwatolea viongozi. Wao walizitolea kwa baba. Na baba walifundisha kweli hizi kwa jamaa zao - leo inafaa baba kufundisha Neno la Mungu kwa watoto wao vivyo hivyo.

Somo: Leo tutasemezana juu ya kfanya chaguo - kitu tunachofanya kila siku.

Asubui ulichagua kwamba badala ya kubaki kitandani utafika kwa darasa. Wengine walichagua kubaki. Ulifanya chaguo gani nyingine leo? (Usaidie watoto kujibu).

Kila mara tunapofanya chaguo, neno linatukia. Maneno mazuri yanatukia wakati tunapochagua vizuri. Maneno mabaya yanaweza kuwa wakati tunapochagua vibaya.

Zamani ilikuwa lazima kwa watu wa Israeli kufanya uchaguo mukubwa. Waliweza kufanya uchaguo muzuri ao uchaguo mubaya. Watachagua nini?

Watu wa israeli walikuwa watu wa pekee wa Mungu. Aliwachagua kwa yeye mwenyewe. Alikuwa na makusudi makubw akwa taifa hili. Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu mwenyewe, atazaliwa ndani ya jamaa moja ya Waisraeli. Mataifa wote wa dunia watabarikiwa kwa yeye. (Ona Mwanzo 12:3). Mungu alitaka sana Waisraeli wamupende na kumutii.

Walikuwa wakikwenda kwa inchi ambayo Mungu aliwaahidi. Mungu alitaka watu wake wakumbuke ya kwamba alikuwa mutawala wao. Hakutaka wasahau yote ambayo aliwafanyia. Hivi tuliona katika masomo mengine kwamba Mungu aliwatolea amri nyngi.

Mungu alitaka watoto na wazazi kufahamu na kutii sheria zake. Hivi Musa alieleza maelezo ya Mungu kwa viongozi. Ilikuwa kazi yao kurudi kwao na kuwaambia jamaa zao yote Mungu aliyooamuru.

Finehasi, kijana mudogo Mwisraeli, angesikiliza kwa uangalifu wakati baba yake alipoeleza kwamba Mungu amefanya agano pamoja nao.

Finehasi aliuliza: "Baba, agano ni nini?"

"Agano ni mpatano, Finehasi. Uwaze kwamba niliahidi kukupa kombeo jipya kama ukikamua ngombe zetu kila siku kwa juma moja. Hili ni agano. Kama ukichunga sehemu yako ya mapatano, utapata kombeo. Kama usipokamua ngombe kila siku, umevunja agano na hutapata kombeo."

1. Maonyo juu ya sanamu (Walawi 26:1-2.)

Baba ya Finehasi aliendelea kusema: "Mungu ameagiza tusiabudu sanamu."

Onyesha taswira 13: Finehasi alikumbuka siku wakati Musa alipokuwa mulimani akisemezana na Mungu Waisraeli walikuwa pasipo saburi, wakaomba Haruni kuwafanyia sanamu. (Ukumbushe wanafunzi neno lililotukia kwa Kutoka 32 kwa njia ya kuwauliza maulizo - Ona Agano la Kale, Kitabu 9, somo 2).

Finehasi aliuliza: "Mungu alitukasirikia siku ile, sivyo baba?"

Baba yake alisema polepole: "Ndiyo. Alikuwa na kasirani hakika, na haikuwa mubaya kwa yeye kukasirika. Sisi tulimwasi, na kusudi, kuabudu sanamu tuliyofanya na mikono yetu. Watu elfu tatu walikufa siku ile kwa sababu ya zambi yetu kubwa."

Finehasi alikuwa kimya, akiwaza ya kwamba ilikuwa neno nzito sana kuasi Mungu.

Baba yake aliendelea kusema: "Watu wengi wanaokaa ndani ya inchi mupya, pahali tunapokwenda, wanaabudu sanamu."

Finehasi aliuliza: "Kwa nini wanaabudu kitu wanachofanya na mikono yao wenyewe? Watu wana uwezo wao wenyewe kuliko sanamu wanazofanya. Namna gani wanaweza kuamini sehemu ya ubao ao jiwe lisiloweza kusikia, wala kuona, wala kuwasaidia?"

Baba yake alijibu: "Kwa sababu hawaamini Mungu wetu aliye hai. Shetani anawapofusha macho. Hawaoni ya kuwa ni upumbavu kuabudu vitu namna hivi. Lakini Mungu anajua kwamba wakati tunapoingia inchi yao, sisi vilevile tutajaribiwa kuabudu sanamu. Anatukumbusha tena na tena ya kwamba Yeye ni Mungu wetu. Anaagiza: 'Musisahau Sabato na Siku za karamu. Musiache Hema na zabihu. Mukumbuke amri zangu. Zitawakumbusha ninyi mambo yote ambayo niliwafanyia ninyi. Halafu hamutajaribiwa kufanya sanamu na kuziabudu.'"

2. Baraka kwa kutii (Walawi 26:3-13; Torati 28:1-14.)

Finehasi aliuliza: "Ile ni sehemu yetu ya agano?"

"Ndiyo, Mungu anatutolea ili tujue namna anavyotaka tumwabud. Amekwisha kueleza namna gani imefaa tuishi kumupendeza. Anatumaini kwamba tunajua sheria hizi na kuzitii."

Finehasi alitaka kujua: "Kisha nini ni sehemu yake ya agano?"

"Ameahidi maneno mengi mazuri kama tukifanya amri zake: (1) Atatuma mvua kwa mashamba yetu. Atatupa vyakula vingi hata vingine vitabaki wakati ni saa kupanda mashamba tena. (2) Vita haitakuwa. Adui watatuogopa. (3) Mungu atafukuza nyama za poli wasiweze kutuzuru. (4) Atatupa sisi watoto wengi.

Onyesha taswira 14: (5) "Na bora kuliko, atakaa katikati yetu katika Hema. Atakuwa Mungu wetu na tutakuwa watu wake. Hatutakuwa watumwa tena kwa mutu yeyote!" Baba alizidi kufurahi wakati aliposema juu ya baraka Mungu alizoahidi.

3. Laana ya kutokutii (Walawi 26:14-39; Torati 28:15-68.)

Finehasi aliuliza: "Nini itatokea kaa tusipotii amri za Mungu?"

Baba alisema kwa upole akiwaza saa nyingi mbele ya kujibu. Alisema kwa heshima: "Ninatumaini haitatokea kamwe. Mungu ametuonyesha hukumu mbaya sana ambayo itatupata kama tusipotii. Ni lazima tusisahau kamwe ya kuwa Mungu ni mwenye haki. Yeye ni mwaminifu kuhukumu zambi kama anavyobariki

utii. Kama tukimwona bule na tuspomusikiliza na kumutii anatuonya kwamba (1) atatuma nzige kula nafaka zetu, (2) hatatuma mvua kwa mashamba yetu. Vitu vyote vitakauka na miti haitazaa matunda. (3) Ataacha adui kututawala. (4) Atatuma ugonjwa mubaya juu yetu. (5) Atatuma nyama za poli kuua watoto wetu na nyama zetu."

Onyesha taswira 15: Baba ya Finehasi aliendelea kusema: "Kama tukiendelea kuabudu sanamu na kusahau siku za karamu na miaka ya kupumzika kwa inchi: (6) Mungu ataacha adui zetu kuja kutupeleka kama wafungwa kwa inchi zao. Tutakuwa mbali na inchi Mungu anayotaka tuwe nayo. Tutatengwa mumoja kwa mumoja. Hatutaishi pamoja kama taifa chini ya utawala wa Mungu. Hatakaa katikati yetu tena katika Hema."

Mungu alifanya agano la heshima kabisa na watu wake!

Ilikuwa kwa Israeli kufaya uchaguo. Uwaze kama ulikuwa pamoja nao wakati walipoingia inchi ya Kanana. Ungechagua nini? (Uache wanafunzi kuzungumuza)

4. Ukosefu wa Israeli na tumaini lao kwa wakati wa kuja (Walawi 26:40-45; Yeremia 23:7-8; 30:3; 31:33-34.)

Mungu alitolea waisraeli uhuru kuchagua nani atakayefuata. (Soma polepole na waziwazi Torati 30:15-20 kwa wanafunzi . Uulize maulizo kujua kwamba wanafahamu)

Ningependa kuwaambia ninyi kwamba Waisraeli walitii Mungu na kufurahi na baraka zake nzuri sana. Lakini Biblia inaandika habari za huzuni. Wakati walipofika inchi ya Kanana, waliasi Mungu. Hawakuharibu watu waovu pale kama Mungu alivyoamuru. (Ona Torati 20:16-18). Lakini waliishi katikati yao. Nyuma kidogo watu Mungu aliochagua kwa yeye mwenyewe walikuwa wakiabudu sanamu zilizofanywa na miti na mawe. Waliabudu miungu ya uwongo. Waza juu yake!

Mungu alikuwa na saburi nao. Alituma manabii kuwaonya. Mara nyingine walisikiliza kwa wakati. Kisaha walisahau. Mia za miaka ilipita. Waisraeli hawakuwaza juu ya sehemu yao ya agano. Mungu hakuweza kusahau zambi yao. Aliendelea kuwaonya, "Kama mukikataa kunitii, mutashindwa na adui zenu. Watawapeleka ninyi kwa inchi ya wageni kuwa watumwa." Ni neno hili lilitokea. Waisraeli waliteswa kwa uchaguzi wao mubaya. Wengi sana waliteswa bila rehema na kuuawa na adui zao.

Hata leo, Waisraeli wansambalana katika kila inchi ya dunia. Mpaka miaka makumi sita mbele, hawakuwa na inchi. Tangu 1948, Wayuda wengi wamekuwa kwa inchi yao wenyewe, Israeli. Lakini wangali wanakataa kuamini Bwana Yesu ni Mwana wa Mungu.

Onyesha taswira 16: Unafikiri Mungu amekwisha kuwasahau? Hapana, hata kidogo! Siku moja wakati Yesu atakaporudi duniani, wengi wao watatubu. Wataingia ufalme wa Kristo atakaosimamisha duniani kwa miaka elfu moja. Bwana atawarudisha kwa inchi yao na kutawala juu yao kwa haki. Yesu atakuwa Mufalme Mukamilifu. Na, kwa mara ya kwanza, dunia hii itakuwa na serkali kamilifu. (Ona Ezekieli 37:21-28)

Itakuwa namna gani duniani kwa muda ule wa miaka elfu moja? Mungu atatuma mvua nyingi hata mavuno yatakuwa makubwa tena. Watu watakaa kwa salama katika inchi yao wenyewe. Wala adui zao wala nyama wakali hawataweza kuwazuru. Watu hawatakuwa na njaa wala ugonjwa. Kila kosa litaazibiwa mara moja na Yesu Kristo, Mufalme. Salma itakuwa kwa dunia yote kwa miaka elfu moja! Itakuwa wakati wa furaha kubwa! (Ona Ezekieli 34:23-31; Isaya 35:5-6; 32:1). "Dunia itajaa na kujua Bwana (Isaya 11:9).

Utakuwa wapi wakati Kristo atakapotawala kwa miaka elfu moja? Kama wewe ni mutoto wa Mungu, utakuwa hapa duniani na kutawala pamoja na Bwana Yesu Kristo kwa wakati ule. (Ona Ufnuo. 20:6). Utachagua kumutii wakati wa sasa? Anataka umufanyie nini juma hili? Ufanye kusudi namna gani utamutii juma hili.

Kama ukikataa kuamini Bwana, utatengwa na Mungu. Kama ukitengwa na Mungu utateswa na hukumu yake katika ziwa na moto kwa milele. Kwa nini? Kwa sababu ulikosa kuchagua Mwana wake, Yesu Kristo, kuwa mwokozi wako. Utakiri zambi zako kwa Mungu sasa hivi na kupokea Kristo kuwa Mwokozi wako?